

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.LDC/L.10/13 VOL.V/04**

**Tarehe. 17/09/2021**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA KWA KUSHIRIKIANA NA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA ANATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III KAMA IFUATAVYO:-**

**MTENDAJI WA KIJIKI III – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 8)**

**1. SIFA ZA KUAJIRIWA**

Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

**2. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote zote za halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za kijiji.
- vii. Kujibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa Njaa, Umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- viii. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi
- ix. Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji
- x. Kuibua vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanyaji wa Mapato katika Kijiji
- xi. Kuandaa na kutunza Rejesta za Wakazi wote katika Kijiji

